RBWB
RUFIJI BASIN WATER BOARD

# Ripoti ya Kihaidrolojia Ya Kila Mwezi (Bwawa la Mtera)


## Aprili (2026)

## 1 Muhtasari wa Hali ya Maji

Bwawa la Mtera hupokea maji kutoka mito mikuu mitatu: Great Ruaha, Little Ruaha na Kizigo, ambayo ni sehemu ya kidakio cha Great Ruaha. Mito hii ni muhimu kwa uzalishaji wa umeme wa maji, kilimo, matumizi ya majumbani na ikolojia.

Katika mwezi wa Aprili 2026, viwango vya maji vilikuwa juu ya wastani kwa asilimia 240 ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu wa mwezi husika. Hali hii ilisababishwa na mvua kubwa katika vidakio pamoja na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji. Aidha, usawa wa maji katika bwawa la Mtera ulikuwa juu kwa asilimia 100.55 ukilinganisha na wastani wa muda mrefu.

Zoezi la upunguzaji wa maji kutoka katika bwawa la Mtera lililoanza rasmi tarehe 31 Machi 2026 linaendelea. Mpaka kufikia tarehe 30 Aprili 2026 jumla ya mita za ujazo billioni 1.34 zimepunguzwa kutoka katika bwawa ili kulinda usalama wa miundombinu ya bwawa.





## 2 Hali ya Hewa

**Hali ya Mvua – Aprili 2026:**
Takwimu za mvua zilizorekodiwa na vituo vya hali ya hewa katika maeneo mengi ya Bonde la Rufiji zilikuwa za wastani hadi juu ya wastani, na hivyo kuongeza mtiririko wa maji katika mito.

***Mwelekeo – Mei 2026:***
Kwa mujibu wa utabiri wa hali ya hewa uliotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA):

- Mvua zitaendelea kunyesha katika wiki ya kwanza na ya pili katika maeneo mengi ya bonde. Hata hivyo, mvua hizi zitakuwa ni kubwa zaidi katika mabonde madogo ya Kilombero, Luwegu na Lower Rufiji kuliko itakavyokuwa upande wa Great Ruaha.
- Wiki ya tatu na ya nne maeneo mengi ya bonde yatapokea mvua chache.





## 3 Hali ya Mtiririko wa Maji

Katika mwezi Aprili 2026, mtiririko wa maji uliendelea kuwa juu kutokana na mvua zilizokuwa zinaendelea kunyesha katika maeneo ya juu ya Bonde la Great Ruaha.

*Jedwali 1: Wastani wa Mitirirko wa Maji Mwezi (Aprili 2026 ) Ukilinganisha na LTA (2000–2025).*

| Na. | Namba ya Kituo | Mto | Wastani Mtiririko wa Maji (m3/s) Aprili 2026 | Wastani Mtiririko wa Maji - LTA (Aprili) 2000-2025 | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1KA59 | Great Ruaha at Msembe | 602 | 113 | Juu zaidi ya Wastani |
| 2 | 1KA31 | Little Ruaha at Mawande | 45 | 44 | Wastani |
| 3 | 1KA42A | Kizigo at Chinugulu | 28 | 33 | Wastani |

Wingi wa maji mitoni katika Mwezi wa Aprili 2026 umeongezaka. Hali hiyo imepelekea bwawa la Mtera kufikia kiwango cha juu cha uzalishaji cha 698.5 masl. Hali hii inapelekea mchakato wa upunguzaji wa maji kuchukua muda mrefu wa takribani siku 31 mpaka kufikia mwisho wa mwezi wa Aprili 2026.





## 4 Viwango vya Maji Bwawani

Katika mwezi Aprili 2026:

- Hali ya Usawa na wingi wa maji katika bwawa iliendelea kuwa juu ya uzalishaji umeme ('Maximum Operational Level kwa takribani siku 30 (Kuazia tarehe 31 Machi 2026 Mpaka 30 Aprili 2026)
- Upunguzaji wa maji katika bwawa unaendelea mpaka sasa ili kulinda usalama wa miundombinu ya bwawa, kupunguza hatari za mafuriko na kuendeleza uzalishaji wa umeme kwa ufanisi.

***Uchambuzi wa Kihaidrologia***

- *Ujazo wa juu wa maji unaimarisha uwezo wa uzalishaji wa umeme.*
- *Mvua zinazoendelea Mei 2026 katika maeneo ya vidakio vya Kilombero na Luwegu zinaweza kuongeza mtiririko wa chini ya mto (downstream) kwa vipindi vichache.*
- *Vipindi vya ukavu vinavyotarajiwa kuanzia wiki ya tatu ya Mei vitapunguza taratibu mtiririko wa maji katika mito.*




## 5 Mapendekezo

- Kuendelea na upunguzaji wa maji ili kulinda usalama wa miundombinu ya bwawa.
- Kusimamia mtiririko wa maji kuelekea maeneo ya chini ya mto kwa kupunguza athari za mafuriko.
- Kuhakikisha kiwango cha maji kinabaki ndani ya viwango vya juu vya uzalishaji umeme ili kuendeleza uzalishaji wa umeme wa maji kwa ufanisi na matumizi mengine ya maji.